Neno La Mungu
(God's Word)

na

Ellis P. Forsman

Neno La Mungu

na

Ellis P. Forsman

Octoba 12, 2011

Neno La Mungu

Luka 4:4

Luka 4:4, "*Yesu akamjibu, imeandikwa ya kwamba mtu hataishi kwa mkate tu.*"

Je ni kweli kwamba Biblia ni neno la Mungu? Majibu ya watu wengi inaweza kuwa, "Ndiyo," kama yalivyo majibu yako pia; lakini unawezaje kuendelea kuthibitisha? Kama ungeulizwa Biblia ilitoka wapi, nani aliiandika, lini na wapi, je ungeweza kutoa jibu la kiintelijensia na linaloshawishi kwa maswali haya?

Kuna watu wengi maelfu wanaipenda Biblia; ni mfariji wao wa kila siku na rafiki. Wamelelewa toka utotoni kuamini kwamba Biblia ni kitabu kisicho na makosa, neno kwa neno limevuviwa.

Walipoitwa ili kutoa sababu ya imani yao katika neno la Mungu, walisema tu kwamba, "*Tumekuzwa ili tuiamini Biblia; baba zetu na mama zetu wanaliamini; na, hivyo basi, tunaliamini, na hatujawahi kuwa na shaka kuihusu.*"

Lakini tunapaswa kuwa na imani zaidi ya imani za kimila katika Biblia. Msingi wa imani kama huo sio tu kwamba inatafakari na haijatulia; inatosha kwa ajili ya majaribu ambayo imani yetu hukumbana nazo.

Kuna kutu kimoja ambacho tuna uhakika nalo – Biblia iko hapa; tunayo. Kweli au si kweli, nzuri au mbaya, imevuviwa au haijavuviwa, inatoka kwa Mungu au wanadamu, iko hapa.

Baba zetu walikuwa nayo kabla yetu; baba zao pia walikuwa nayo, pia. Waliipata wapi?

Tuangalie baadhi ya ukweli kuhusu neno la Mungu:

Neno La Mungu Limevuviwa

Kwa sababu inaonekana.

Hii inaonekana kutokana na ilikotoka.

Vitabu vingi vya wanadamu ni matoleo ya mtu mmoja au wachache. Haiku hivyo kwa Biblia, kwa sababu iliandikwa na watu arobaini, waaliokuwa wakiongozwa na Roho Mtakatifu.

Biblia ni binadamu. Vitabu hivi vimepitia akili za wanadamu; zimeandikwa kwa lugha za kibinadamu; ziliandikwa na kalamu kwa mikono ya wanadamu.

Alafu, Biblia ni ya Kimungu. Kuna vitabu vingine vizuri duniani, lakini hakuna hata kimoja utaakacho linganisha na hiki, kwa sababu ni zaidi ya toleo la binadamu, ni ya Kimungu.

Hii pia huonekana katika utunzwaji wake.

Neno la Mungu lilipitishwa katika nyakati nyingi za mateso, alafu bado, imezuia kila shambulizi la hao ambao wangeweza kuiharibu. Mat. 24:35, "*Mbingu na nchi zitapita, lakini neno langu halitapita.*"

Hii pia huonekana katika mzunguko wake.

Imekwenda katika lugh nyingi. Baada ya miaka 1900 Maandiko yapo katika lugha 210 katika Biblia yote, na katika lugha 270 tofauti ya Agano Jipya; ndiyo taarifa inayotolewa na Chama cha Biblia cha Amerika.

Ipo katika matole mengi. Chama cha Biblia cha Amerika pekee hutoa zaidi ya nakala milioni za Biblia kwa mwaka.

Kwa sababu inadai kuwa imevuviwa.

(Madai haya yanatokea katika Maandiko yote).

Katika Agano La Kale.

- Vitabu vitano vya kwanza – Hapa tunapata maelezo mengi, kama Bwana alivyosema." (Mwa. 3:9; 6:13; 12:1; 35:1; Kut. 13:1; 20:1).
- Vitabu vya historia – Hapa pia tunapata maelezo yanayofanana kama ya hapo juu. (Yosh. 1:1; 8:1; 1 Sam. 3:1; Fal. 9:2-3; Fal. 23:14).

- Vitabu vya simulizi – Hapa pia tunapata maelezo yanayofanana. (Ayu. 1:7; 2:3; 38:1; Zab. 50:1).
- Vitabu vya Unabii – Mara nyingi katika vitabu hivi tunasoma maneno yanayovutia kama vile "Bwana amenena." (Isa. 1:2; 6:7; Yer. 1:4; Eze. 1:3; Hosea 1:1; Amos 2:1; 3:1; Yon. 1:1).

Katika Agano Jipya.

Hapa kuna vifungu vingi vinavyoshuhudia kwamba Biblia imevuviwa.

- Injili nne. Yohana 14:24, "*Mtu asiyenipenda yeye hayashiki maneno yangu; nalo neno mnalolisikia silo langu, ila ni lake Baba aliyenipeleka.*"
- Matendo ya Mitume
  - Mdo. 2:16, "*Lakini jambo hili ni lile lililonenwa kwa kinywa cha nabii Yoeli,*"
  - Mdo. 2:25, "*Maana Daudi ataja habari zake, nalimwona Bwana mbele yangu siku zote, kwa yuko upande wa mkono wangu wa kuume, nisitikisike.*"
  - Mdo. 2:33-35, "*Basi yeye akiisha kupandishwa hata mkono wa kuume wa Mungu, na kupokea kwa Baba ile ahadi ya Roho Mtakatifu, amekimwaga kitu hiki mnachokiona sasa na kukisikia. Maana Daudi hakupanda mbinguni; bali yeye mwenyewe anasema, Bwana alimwambia Bwana wangu, keti upande wa mkono wangu wa kuume. Hata nitakapowaweka adui zako chini ya miguu yako.*"
- Nyaraka.
  - 1 Kor. 2: 12-13, "*Lakini sisi hatukuipokea roho ya dunia, bali Roho atokaye kwa Mungu, makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu. Nayo twayanena si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu, bali yanayofundishwa na Roho, tukiyafasiri mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni.*"

- 1 Kor. 14:37, "*Mtu akijiona kuwa ni nabii, au mtu wa rohoni, na ayatambue hayo ninayowaandikia, ya kwamba ni maagizo ya Bwana.*"
- 1 Thes. 2:13, "*Kwa sababu hiyo sisi nasi twamshukuru Mungu bila kukoma, kwa kuwa mlipopata lile neno la ujumbe la Mungu mlilolisikia kwetu, mlilipokea si kama neno la wanadamu, bali kama neno la Mungu; na ndivyo lilivyo kweli kweli; litendalo kazi pia ndani yenu ninyi mnaoamini.*"

- Ufunuo wa Yohana. Ufu. 22:18-19, "*Namshuhudia kila mtu ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabu hiki, mtu yeyote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki. Na mtu yeyote akiondoa lo lote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima, na katika ule mji mtakatifu ambao habari zimeandikwa katika kitabu hiki.*"

Kwa sababu <u>inathibitisha</u> kuwa imevuviwa.

Hii inaonekana katika utimizaji wa unabii wake.

Chukulia kwamfano, unabii kuhusu Babeli. Isaya 13:14-22, "*Basi itakuwa kama vile paa aliyetishwa, na kama vile kondoo wasio na mtu wa kuwakusanya; kila mtu atageukia watu wake; nao watakimbia kila mtu aende nchi yake mwenyewe. Kila mtu atakayeonekana atatumbuliwa, na kila mtu atakayepatikana ataanguka kwa upanga. Na watoto wao wachanga wata vunjwavunjwa mbele ya macho yao, nyumba zao zitatekwa nyara, na wake zao watatendwa jeuri. Tazama nitawaamsha Waamedi juu yao ambao hawaoni fedha kuwa kitu, wala hawafurahii dhahabu. Na nyuta zao zitawaangusha vijana; wala hawatahurumia mazao ya tumbo; jicho lao haalitawahurumia watoto. Na Babeli huo utukufu wa falme, uzuri wa kiburi cha Wakaldayo, utakuwa kama Sodoma na Gomora hapo Mungu alipoiangamiza. Hautakaliwa na watu tena kabisa, wala watu hawatakaa ndani yake tangu kizazi hata kizazi. Mwarabu hatapiga hema yake huko, wala wachungaji hawatalaza makundi yao huko. Lakini huko watalala hayawani*

wakali wa nyikani; na nyumba zo zitajaa bundi; mbuni watakaa huko; na majini watacheza huko. Na mbwa-mwitu watalia ndani ya ngome zake; na mbweha ndani ya majumba ya anasa; na wakati wake u karibu kufika, na siku zake hazitaongezeka."

Kwamba Biblia inajithibitisha yenyewe kwamba imevuviwa pia inaonekana katika umoja wake wa ajabu.

Umoja wa Biblia unaonyesha umoja wa uhariri. Tunaongelea Biblia kama kitabu, kiuhalisia, ndivyo ilivyo; lakini ni mkusanyiko wa vitabu sitini na sitaa, ikiandikwa kwenye kusudi moja – uhusiano wa mwanadamu kwa Mungu.

Kwamba Biblia inajithibitisha yenyewe kuwa imevuviwa inaonekana katika uajabu usiopimika wa ufundishaji wake kuliko vitabu vingine au vitabu vyote.

Inaonekana kuwa ni mtindo wa siku kwa wenye wasiwasi wa siku zetu kulinganisha mafundisho ya Biblia na yale ya wanafilosofia wa dunia iliyopita, kama Pilato, Aristotle, Socrates, na wengine.

Lakini yeyote anayeweka maandishi haya katika kiwango hicho kinachofanana na Biblia lazima awe amekaidi mafundisho ya Biblia, au amekaidi mafundisho ya watu, au vyote.

Neno La Mungu linamamlaka

Twende kwa nani kwa ajili ya mamlaka ya dini?

Yesu alisema katika Mat. 28:18, "*Yesu akaja akawaambia, nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani.*"

Uwezo: mamlaka, hii hutuliza la mamlaka katika Ukristo. Yesu ana mamlaka <u>yote.</u> Hii haimpi Musa mamlaka, Daudi; hakuna mamlaka kwa ajili ya Joseph Smith, au E. G. White, au Baker Eddy; hakuna mamlaka kwa ajili ya washauri na makundi ya watu.

Kwa nini tunapokea Biblia kama mwongozo wetu pekee wa imani na matendo?

Kwa sababu tulipewa kwa kusudi lilo hilo.

- Mat. 7:21, "*Si kila mtu aniambiaye Bwana, Bwana, atakayeingiaa katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu wa mbinguni.*"
- Mat. 7:24-27, "*Basi kila asikiaye hayo maneno yangu na kuyafanya atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba, mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile isianguke; kwa maana misingi yake imewekwa juu ya mwamba. Na kila asikiaye hayo maneno yangu asiyafanye, atafananishwa na mtu mpumbavu, aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga; mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, ikaanguka; nalo anguko lake likawa kubwa.*"
- Luka 10:16, "*Awasikilizaye ninyi anisikiliza mimi, naye awakataaye ninyi anikataa mimi; naye anikataaye mimi amkataa yeye aliyenituma.*"

Kwa sababu agizo la kipekee haina kosa.

- Zab. 19:7, "*Sheria ya BWANA ni kamilifu huiburudisha nafsi, huiburudisha nafsi. Ushuhuda wa BWANA ni amani, humtia mjinga hekima.*"
- 2 Tim. 3:16-17, "*Kila andiko lenye pumzi ya Mungu lafaa kwa mafundisho na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, kwa kuwadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema.*"

Neno la Mungu linanguvu

Mvuto wake juu ya dunia iliyoendelea.

Bila shaka, imekuwa kiunganishi katika dunia yenye mvuto wa kimaendeleo.

Chukulia kwa mfano, kazi ya upaji rangi. Kazi ya mpaka rangi mkuu yote inaonyesha mvuto ambao Biblia imeweka katika nyanja hii: Da Vinci "Chakula cha Mwisho," Ya Raphael "Sistine Madonna," na "Kubadilika sura," na Michelangelo "Musa." Wote hao wanamiliki walipotoka kwenye Biblia.

Chukulia kwa mfano, uwanja mkubwa. Michezo mingi mikubwa ya leo imetokana na uvivio wao katika Biblia. “Mfalme wa Wafalme,” “Malisho Mazuri” na “Amri Kumi” yote yalivuviwa na Biblia.

Chukulia kwa mfano, ulimwengu wa mziki. Wapiga mziki wakubwa kama vile Bach, Handel, Mendelssohn, Mozart, na Beethoven; wote wanapokea uvuvio wao zaidi kutoka katika Biblia.

Ni nguvu inayobadilisha.

Kuna nguvu kubwa inayobadilisha na kuongoa mtu binafsi kuwa katika maisha ya mwanadamu mzuri akiinuliwa na Mungu na neno lake. Hakuna kitabu kingine kilicho na uwezo unaoshinda nguvu ambayo Biblia inayo.

Ni nguvu inayofariji.

Haijawahi kutokea na wala haitakuwepo chanzo chochote ambayo inaweza kuleta faraja kwa mioyo inayo huzunika kama iliyonayo neno la Mungu. (Vifungu vingi katika Biblia yote yanaweza kunukuliwa katika matukio mengi.)

Neno La Mungu Haliaribu

Ni ukweli usiopingika kwamba kile ambacho mwanadamu anaweza kutengeneza, pia mwanadamu uyo huyo anaweza kuharibu. Kwa nini basi, kama Biblia imetengenezwa na mwanadamu tu wa kawaida, ana karne kumi na tisa ya shambulio juu ya Biblia wameshindwa kuiangamiza.

Wakristo wanaamini kwamba Biblia ni neno Takatifu la Mungu ambayo haiwezi kuangamizwa.

- Zab. 119:89, “*Ee BWANA neno lako la simama imara mbinguni hata milele.*”
- 1 Pet. 1:24-25, “*Maana mwili wote ni kama majani, na fahari yake yote ni kama ua la majani. Majani hukauka na ua lake huanguka; bali neno la Bwana hudumu hata milele. Na neno hilo ni neno lile jema lililohubiriwa kwenu.*”

Hitimisho

Mungu hajaivuvia pasipo sababu, kuifunua, kuiandika na kutunza neno lake. Iliandikwa kwa kusudi kwamba "*tuamini kwamba Yesu ni Kristo, Mwana wa Mungu, na kuamini huko mpate kuwa na uhai ndani yenu.*" (Yoh. 20:31).

Hivyo basi, tuwe na mioyo iliyonyenyekea kusikia neno lake, kutii maagizo yake yote, na kwa uwezo wake tuzae matunda ya Roho katika maisha yetu. Jifunze Biblia kila siku, jifunze kimaombi na utii. Tembea nuruni katika mwangaza wake na uokolewe mwishoni kwa uwezo wake.